TANGAZO LA SERIKALI Na. 18 la tarehe 3/1/2025

SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI
(SHERIA NA. 1 YA MWAKA 2024)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 49(2))*

NOTISI YA KUWEPO KWA NAFASI WAZI YA KITI CHA UBUNGE KATIKA JIMBO LA KIGAMBONI YA MWAKA 2025

Sheria Na. 1 ya 2024

KWA KUWA, kifungu cha 49(2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani kinampa Spika wa Bunge la Tanzania mamlaka ya kutangaza nafasi ya Ubunge pale Mbunge anapojiuzulu, anapofariki dunia au anapoachia nafasi ya ubunge kwa sababu nyingine tofauti na zilizoainishwa chini ya kifungu cha 142 cha Sheria hiyo;

NA KWA KUWA, Mhe. Dkt. FAUSTINE ENGELBERT NDUGULILE aliyekuwa Mbunge, Jimbo la Kigamboni aliyedhaminiwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) alifariki dunia tarehe 27 Novemba, 2024;

Sheria Na. 1 ya 2024

KWA HIYO SASA, mimi Dkt. TULIA ACKSON, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mamlaka niliyopewa chini ya kifungu cha 49(2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ninautaarifu umma kama ifuatavyo:

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kuwepo kwa Nafasi Wazi ya Kiti cha Ubunge katika Jimbo la Kigamboni ya mwaka 2025.

Tangazo

2. Kiti cha Ubunge wa Jimbo la Kigamboni kinatangazwa kuwa kipo wazi.

Dodoma
2 Januari, 2025

TULIA ACKSON,
*Spika*